

Zabuni Na. KCU/Z/2023/2024/13

05.04.2024

MWALIKO WA ZABUNI YA USHAURI WA UJENZI KUFANYA UJENZI WA MADUKA KUZUNGUKA VIWANJA NO 7,9 NA 11 VILIVYOPO ZAMZAM BUKOBA MANISPAA

1. Kagera Co-operative Union (1990) LTD imetenga fedha ya kwa ajili ya kujenga maduka kuzunguka viwanja No 7,9 na 11 vilivyopo Zamzam Bukoba Manispaa.
2. Mkandarasi Mshauri ambaye amesajiriwa na anayetambulika na Bodi (AQRB) anatakiwa kuleta maombi ya kiufundi yaani **profile** ya kampuni, kazi alizokwisha fanya, uwezo wa watumishi alionao wa kufanya kazi hii na sifa nyinginezo (technical proposal) pamoja na makisio ya kifedha (financial proposal). Juu ya bahasha ya kiufundi paandikwe "**Maombi ya ushauri wa kiufundi**" na juu ya baasha ya kifedha paandikwe "**maombi ya kifedha**"

Aidha, bahasha ya maombi ya kiufundi na bahasha ya makisio ya kifedha yaliyofungwa vizuri yawekwe katika bahasha moja na juu ya bahasha hiyo paandikwe:-

"ZABUNI YA USHAURI WA UJENZI KUFANYA UJENZI WA MADUKA KUZUNGUKA VIWANJA NO 7,9 NA 11 VILIVYOPO ZAMZAM BUKOBA MANISPAA". Bahasha ziletwe kwa mkono na kumkabidhi Afisa manunuzi kabla ya tarehe 12.04.2024 saa 4.00 asubuhi siku ya Ijumaa kwa anuani hii:-

**MENEJA MKUU,
KCU (1990) LTD,
P.O.BOX 5,
BUKOBA**

3. Ufunguzi wa bahasha utafanyika katika ukumbi wa mikutano wa KCU (1990) LTD mara tu baada ya muda wa kuleta maombi kuisha yaani tarehe 12.04.2024 saa 4.00 asubuhi siku ya Ijumaa. Waombaji mnakaribishwa kuhudhuria ufunguzi huo.
4. Mwombaji atakaye hitaji ufanuzi zaidi kuhusu zabuni hii awasiliane na ofisi ya Ardhi nyumba na uwekezaji KCU (1990) LTD.
5. Mwombaji anatakiwa kufika katika ofisi ya Afisa Manunuzi kwanzia saa 2.00 asubuhi hadi saa 10.00 mchana siku za kazi kwa ajili ya kupewa nyaraka ya zabuni (**tender documents**).
6. Siku ya kutembelea eneo la ujenzi (Site visit) ni tarehe 09.04.2024 saa 4.00 asubuhi siku ya Jumanne, na safari itaanzia KCU makao makuu.

7. Maombi yatakayoletwa kwa kucheleta, maombi ya kieletroniki na maombi ambayo hayajufunguliwa katika sherehe ya ufunguzi hayatapokelewa kwa ajili ya kufanyiwa tathmini.

Imetolewa na:

**MENEJA MKUU
KAGERA CO-OPERATIVE UNION (1990) LTD**

